TANGAZO LA SERIKALI Na. 9 La Tarehe 13/1/2023

SHERIA YA MASHIRIKA YA UMMA,

(SURA YA 257)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 38(1))*

AMRI YA KUTAMKA MASHIRIKA YA UMMA KUWA CHINI YA UANGALIZI YA MWAKA 2023

KWA KUWA, Msajili wa Hazina katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa kifungu cha 22 cha Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura ya 257 ametoa mapendekezo kwa Waziri wa Fedha kwamba baadhi ya Mashirika ya Umma kutamkwa kuwa Mashirika ya Umma Yaliyochini ya Uangalizi; na

NA KWA KUWA, kifungu cha 38(1) cha Sheria hiyo kinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha kwa Amri iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali kutamka Shirika la Umma kuwa Shirika la Umma Lililo Chini ya Uangalizi;

HIVYO BASI, Mimi MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU, Waziri wa Fedha na Mipango, katika kutekeleza mamlaka niliyopewa na kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura ya 257, natoa Amri ifuatayo:

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutamka Mashirika ya Umma Kuwa Chini ya Uangalizi ya Mwaka 2023.

Tamko la mashrika ya umma kuwa chini ya uangalizi Sura ya 257

2. Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii yanatamkwa kuwa chini ya uangalizi na masharti ya Sheria ya Mashirika ya Umma yatatumika kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa Amri hii.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

1. Kilimanjaro Paddy Hauling Company Limited.
2. Polysacks Company limited.
3. NMC Isaka Rice Mill Complex.
4. Multipurpose Oil Seed Processing Company Limited.
5. CDA Intergrated Concrete Industry Limited.
6. NMC Tabora Rice Mill Complex.
7. Musoma Textile Limited.
8. NMC Mzizima Maize Mill.
9. Pesticides Manufacturers Limited.
10. Manawa Ginneries Company Limited.

Dodoma,
30 Desemba, 2022

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha na Mipango*